THE GUARDIAN JAN 11, 2021



Livestock and Fisheries deputy minister Pauline Gekul (3rd-L) feeds fish during a visit to the Fisheries Education and Training Agency at Mbegani in Bagamoyo District at the weekend. Photo: Correspondent Mbaraka Kambona

Scanned with CamScanner

Nane>> Idadi ya meli za uvuvi zitakazonunuliwa na serikali

## Silinde awaonya watumishi watakaotafuna fedha za miradi

Na SEIF TAKAZA, IRAMBA

SERIKALI imesema haitamfumbia macho mtumishi yeyote wa umma atakayefanya ubadhirifu wa fedha za miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, wakati wa ziara ya siku moja ya kukagua shughuli za miradi ya elimu wilayani Iramba, mkoani Singida.

Silinde, alisema ni jukumu la kila mtumishi wa umma, kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu kwa mujibu wa maadili ya kazi huku akiwataka kuepuka ubadhirifu na hujuma ya kukwamisha miradi ya maendeleo.

"Serikali ya Rais Dk. John Magufuli, imetoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali kwa maendeleo ya wananchi wake, hivyo haitamfumbia macho mtumishi

# Naibu Waziri aagiza chuo kizalishe manahodha wengi meli za uvuvi

NA MWANDISHI WETU

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameutaka Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), kuongeza kasi ya kuzalisha wataalamu watakaokuwa na uwezo wa kuendesha meli za uvuvi wa bahari kuu zitakazonunuliwa na serikali ili kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi kupitia uchumi wa bluu.

Gekul, alitoa kauli hiyo alipofanya ziara katika ofisi za wakala huo, zilizopo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema mpango wa serikali katika miaka mitano chini ya uongozi wa Rais Dk. John Magufuli, ni kununua meli nane zitakazotumika kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu, hivyo ni muhimu kuongeza kasi ya kutoa wataalamu watakaoziendesha meli hizo pindi zitakapofika.

Aliongeza kuwa mwishoni mwa mwaka huu, meli ya kwanza itakuja, huku akisema haitapendeza kama vyombo hivyo vitakuja halafu pasiwepo na vijana watakaohusika na kuviendesha.

"Nchi inawategemea mtoe wataalamu watakaosaidia kuendesha meli hizo zitakazoletwa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, tunaomba mkatuzalishie wataalamu, ambao hatutapata upungufu wa wataalamu wa kuendesha vyombo hivyo," alisema.

Awali, akimkaribisha Naibu Waziri, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Dk. Semvua Mzighani, alisema wameshaingia mkataba wa maridhiano wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutoa vyeti kwa manahodha wa meli, maofisa wa meli, mabaharia na waangalizi wa meli zitakazofanya kazi katika uvuvi wa bahari kuu.

"Huwezi kuajiriwa kule kama hauna cheti cha kukutambulisha, hivyo kupitia maridhiano haya, mabahari watapatikana kutoka katika chuo hiki," alisema.

Dk. Mzighani, aliongeza kuwa kwa Afrika, vyuo vinavyotoa mafunzo kwa wataalamu hao vipo Afrika Kusini na Misri, huku akisema ni wakati mzuri kupitia mafunzo yatakayotolewa hapa nchini, kuongeza ajira kwa vijana na kupata fedha za kigeni kupitia watu kutoka nchi nyingine watakaokuja kusoma katika chuo hicho.

Alisema licha ya mipango na mikakati mizuri waliyonayo katika kuboresha huduma zao, bado wanakabiliana na changamoto kubwa ya gharama za uendeshaji wa vyuo vya uvuvi, hivyo aliiomba serikali iwaongezee nguvu ili watoe wataalamu wazuri, watakaokwenda kulisaidia Taifa kukuza na kuimarisha uchumi wa bluu.

Scanned with CamScanner

FA

# FETA watakiwa kuzalisha wataalamu uvuvi bahari kuu

**Na Mbaraka Kambona,**
BAGAMOYO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameutaka Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kuongeza kasi ya kuzalisha wataalamu watakaokuwa na uwezo wa kuendesha meli za uvuvi wa bahari kuu zitakazonunuliwa na serikali ili kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi kupitia uchumi wa bluu.

Gekul alitoa kauli hiyo alipofanya ziara katika ofisi za wakala zilizopo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Alisema mpango wa serikali katika miaka hii mitano chini ya uongozi wa Rais, Dk. John Magufuli ni kununua meli nane zitakazotumika kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu na kwamba ni muhimu kuongeza kasi ya kutoa wataalamu ambao wataziendesha meli hizo zitakapofika.

Aliongeza kuwa mwishoni mwa mwaka huu meli ya kwanza itakuja na kuwa haitapendeza kama vyombo hivyo vitakuja halafu pasiwapo na vijana watakaohusika na kuviendesha.

"Nchi inawategemea mtoe wataalamu watakaosaidia kuendesha meli hizo zitakazoletwa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, tunaomba mkatuzalishie wataalamu ambao wataendesha vyombo hivyo," alisema Gekul.

Awali akimkaribisha Naibu Waziri, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, FETA, Dk. Semvua Mzighani, alisema wameshaingia mkataba wa maridhiano wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995 na hiyo itasaidia kutoa vyeti kwa manahodha wa meli, maofisa wa meli, mabaharia na waangalizi wa meli zitakazofanyakazi katika uvuvi wa bahari kuu.

"Huwezi kuajiriwa kule kama hauna cheti cha kukutambulisha, hivyo kupitia maridhiano haya sasa mabahari watapatikana kutoka katika chuo hiki," alisema Dk. Mzighani.

Vile vile, alisema kwa Afrika vyuo vinavyotoa mafunzo kwa wataalamu hao vipo Afrika Kusini na Misri na kuwa ni wakati mzuri sasa kupitia mafunzo yatakayotolewa nchini kuongeza ajira kwa vijana na kupata fedha za kigeni kupitia watu kutoka nchi nyingine watakaokuja kusoma katika chuo hicho.

Dk. Mzighani alisema pamoja na mipango na mikakati mizuri waliyonayo katika kuboresha huduma zao bado wanakabiliana na changamoto kubwa ya gharama za uendeshaji wa vyuo vya uvuvi na kuiomba serikali iwaongezee nguvu ili waweze kutoa wataalamu wazuri watakaokwenda kulisaidia taifa kukuza na kuimarisha uchumi wa bluu.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, akiwapa chakula samaki alipotembelea Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), kampasi ya Mbegani iliyopo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Kulia ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Dk. Semvua Mzighani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Scanned with CamScanner

Email: jamvilahabari @gmail .com



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul akiwapa chakula Samaki alipotembelea Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), Kampasi ya Mbegani iliyopo Wilayani Bagamoyo, Mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Kulia kwake ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala hiyo, Dk. Semvua Mzighani

Scanned with CamScanner

...Social Security Fund. Photo: Guardian Correspondent

receiving information from the

miss the essential commodity.

# TALIRI plans to install Centre for Dairy Excellence in Tanga Region

By Correspondent Valentine Oforo, Dodoma

THE Tanzania Livestock Research nstitute (TALIRI) is set to install enter for Dairy Excellence (CDE) n Tanga Region to help improve erformance of the crucial socio-conomic sector in the country, specially milk production.

The robust project, set to start ith a seed capital of at least 424bn/- is projected to serve as a nique demonstration center for airy farmers to embrace best dairy nimal technologies and practices.

Acting General Director for ALIRI, Dr Jonas Kizima, yesterday old the publication that the Institute as in talks with the government f Ireland for availability of the needed seed capital amount, saying however the talks were at impressive stages, added that other funds for the timely initiatives was expected to be sourced from the government of Tanzania.

"However, doors are open for stakeholders from within and outside the country to chip-in and invest in order to allow the project to be furnished with the best-ever technological facilities and services," Dr Kizima expressed.

He stated, the core focus is to enable the dairy farmers in the eastern zone region of Tanga, Dar es Salaam and Coastal to heighten their milk production levels by adopting cattle with good dairy animal genetics, but also, embracing key other practices.

The TALIRI's chief boss itemized some of the key dairy technologies the envisaged center will have in offing as best animal health services, animal compounded and feeds, animal husbandry infrastructure, milk handling, grazing systems and good dairy animal genetics, among others.

"We aspire to develop the center in a professional manner to be a major Demonstration Dairy Farm Center (DDFC) for all dairy farmers within the country. Moreover, the center will also be used to offer dairy tourism to different foreigners that will be touring in the country," he insisted.

Besides, he unveiled that among others, the state-owned institution has decided to install the crucial dairy facility in the region with an eye to help the Tanga Fresh Ltd industry to process milk at its full capacity.

According to him, the famous factory's daily milk processing capacity was at least 120,000 liters, but due to poor supply of milk from dairy farmers the facility was only processing between 50,000 and 80,000 liters.

"The other reason is that Tanga stands tall among regions within the country with many dairy cooperatives and smallholder dairy farmers hence placing the facility there will assist them improving their daily executions, the move which will automatically manage the factory (Tanga Fresh Ltd) to start receiving needed fresh milk for processing," he added.

As the government is working tirelessly to industrialise the country's economy by 2025, he said the institute in its side will run a diverse professional initiative to help improve performance of milk factories, possibly through increasing home milk production, the move which will also curtail milk importation.

Statistics from the Tanzania Dairy Board (TDB) depicts that during 2019/20, the country produced 3.01 billion liters of milk, out of which, 2.1 billion liters was produced from domestic dairy cows and 0.1 billion liters was from hybrid dairy cows.

However, Assistant Registrar of TDB, Noel Byamungu, said the milk produced in the country is still not reflecting the country's actual demand, hence propelling the country to import milk from other countries.

For instance, he said during 2017/18, Tanzania imported 20,920,537.58 LMEs Kg valued at 30,290,485,222/- and during 2018/19 the importation rate stood at 617,448,655Kg.

However, due to advancement of the UHT technology in Tanzania the country's Liquid Milk Equivalent (LME) importation has kept on declining.

However, record proves that Tanzania has successfully managed to increase the number of crossbred dairy cattle at the national level 3.8 times from 783,000 in 2017/18 to 1,294,882 in 2018/19, the development which witnessed the country's milk production expanding from 2.4 to 2.7 billion liters.

HAPPY NEW YEAR
Rate of interest on Savings Accounts
W.E.F 01/01/2021
TZS 3%
USD 1%

# The Guardian

www.ippmedia.com

pestguard
Hygiene Products and Services
Prevention is Better than Cure
Hand Sanitisers, Disinfecta
Tissues Dispensers & Tow
+255 658 781 861
www.pestguard.co.

theguardiantz theguardianltd The Guardian Digital +255 745 700 710 LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 - 5422 ISSUE No. 8109 • PRICE: Tsh 1,000, Kenya sh100 TANZANIA MONDAY 11 JANUARY, 2

**National Pg 3**
Govt orders Ilala to pay contractor



**National Pg 4**
Public servants to plant trees



**National Pg 5**
TFS to distribute tree seedlings



**National Pg 6**
'Employ graduate engineers'



Scanned with CamScanner

# Gekul: Feta nataka wataalamu meli za uvuvi

MWANANCHI JAN 11, 2021

**Bakari Kiango, Mwananchi**
bkiango@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul ameitaka Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (Feta) kuongeza kasi ya kuzalisha wataalamu watakaokuwa na uwezo wa kuendesha meli za uvuvi wa bahari kuu zitakazonunuliwa na Serikali.

Gekuli ambaye ni mbunge wa Babati Mjini alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi kupitia uchumi wa bluu.

Taarifa hiyo iliyotolewa na wizara hiyo inaeleza kuwa Gekul alieleza hayo juzi wakati wa ziara yake katika ofisi hizo zilizopo Bagamoyo mkoani Pwani.

Gekul alisema mpango wa Serikali katika miaka mitano ni kununua meli nane zitakazotumika kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu, hivyo ni muhimu kuongeza kasi ya kutoa wataalamu watakaoweza kuendesha meli hizo zitakapowasili.

"Mwisho wa mwaka huu meli ya kwanza itawasili, haitapendeza kama vyombo hivyo vitakuja halafu hakuna vijana wenye ujuzi wa kuviendesha.

"Nchi inawategemea mtoe wataalamu watakaosaidia kuendesha meli hizo zitakazoletwa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu. Tunaomba mkatuzalishie wataalamu ili tusipate usumbufu wa kuviendesha vyombo hivyo," alisema Gekul.

Ofisa Mtendaji Mkuu Feta, Dk Semvua Mzighani alisema wameshaingia mkataba wa maridhiano wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995.

Scanned with CamScanner